

Utamaduni wa Kiswahili: Wilaya ya Kusini-Unguja

T.S.Y. SENGO

University of Dar-es-Salaam, Tanzania

0.0 HODI - KARIBU: HODI - HODI : KARIBU : STAREHE.

Hadi hivi sasa, kitabu pekee ambacho kimeandikwa kuhusu UTAMADUNI WA WASWAHILI ni kitabu cha Ireri Mbabu¹ wa Chuo Kikuu cha Kenyatta. Juu ya gamba la kitabu hicho, Mbabu anaueleza upeo wa jitihada zake kuwa kazi yake imekusudiwa wanafunzi wanaosomea shule za upili nchini Kenya. Ama, Utamaduni unahuusu mila, asili, jadi, na desturi za mavazi, vyakula, imani, tabia, na maisha ya jamii kwa jumla. Mwalimu Mbabu anasisitiza katika kuwaaidhi wanafunzi wake kwamba utamaduni ndio msingi wa fasihi.

Sura nane za kitabu hicho zimeeleza mengi juu ya *Waswahili* wa mwambao wa Kenya, Uislamu ukipewa nafasi ya kipekee katika maana ya Msahili. Malezi ya Kiswahili yameelezwa kutilia sana mkazo dhana ya heshima katika mapana yake. *Vyuo vya Kurani na Maulidi na Kumbini* ni taasisi mbili zilizoelezea makuzi na malezi ya Kiswahili. *Kazi ya Waswahili* ni pamoja na uvuvi, ukwezi, ukulima, usafiri wa baharini, biashara, ufundi mbalimbali pamoja na uundaji wa vyombo vya bahari n.k. Kazi ya uvuvi imepewa maelezo mengi kwa kuwa ina uzito wa kipekee katika maisha ya Waswahili. Kwa mfano, mitego ya samaki aliyoipata mtafiti ni pamoja na thasi, sonyi, lasha, - mitego hii yote ya majarifa hutumika sana usiku. Uzio ni aina ya pili. Aina ya tatu ni nyavu za mikono. Shipi ni aina ya nne. Bunduki-mshale maalumu wa kupigia samaki baada ya kupiga mbizi majini. Kimia ni aina ya sita. Kuvua kuna vyombo na nyakati zake pamoja na itikadi na mbinu mbalimbali.

Ndoa na Harusi: Uswhilini ni taasisi ya kwanza kwa uzito wa maisha ya kila siku ya mtu. Ubikira ni ada kubwa sana kwa wasichana wa Kiswahili kabla ya kuolewa kwani ndoa ndicho kitovu cha maisha ya Waswahili. Ni desturi iliyoenea mwote Uswhilini, kwa wazazi kuwa washauri wakuu wa ndoa za watoto wao. Kuna hatua kadha wa kadha tangu mtu aposapo hadi kutoa mahari na kufunga harusi. Chuo hicho huwashirikisha makungwi na masomo katika kuwaelekeza na kuwafundisha wari harusi kabla na baada ya harusi. Kwa waumini wa kweli wa Uislamu sharia za Kiislamu huwa ndicho kigezo pekee cha kuendeshea maisha ya ndoa.

¹ Ireri Mbabu, *Utamaduni wa Waswahili*. Nairobi:Kenya publishing & Book Marketing Co. Ltd. 1985.

Mazishi: ni taasisi ya kuwarejesha waja walikotoka, ama na kuwakumbusha walio hai juu ya marejeo hayo kwa Mola wao. Msiba wa Kufiliwa huwa ni faradhi-kifaya kwa Waislamu wote wa ujiranini. Huzuni za kufiliwa huwa ni za wote na kazi kubwa ya majirani na marafiki ni kuwafariji wanandugu waliofiwa. Kazi zote, tangu utoaji wa habari za kifo, uchimbaji ufu, uoshaji, uchimbaji kaburi, kupatikana kwa tusi, uchukuaji wa jeneza, uzikaji na salla zote za kumsalia maiti ni za jumuiya. Watu wote jumuiani lazima wahusike kwa namna moja au nyingine. Huzuni ya kifo, kwa msingi huchukua siku arubaini. Baada ya hapo hufuata ada ndogo ndogo za duaa na kufyagilia mavani kila mara na kila mwaka, daima.

Ushirikina: ni sura ya mwisho katika kitabu cha Mbaabu. Waandishi wengine wangeweza kuiita sura hii *Itikadi*. Yeye ameanza sura yake na taarifa ya jumla juu ya Ushirikina. Ameonesha kuwa jambo hili si la Waswahili tu bali ni la watu wote hata Wazungu na si la Waislamu tu bali ni la Wakristo pia. Itikadi ni taasisi iliyo hai katika tamaduni za jamii zote za wanadamu. Ushirikina ni sehemu ndogo katika itikadi za watu. Uislamu na Ukristo hazifunzi wala kuhimiza itikadi hii. Lakini baadhi ya waumini hujikuta wamejaa tele ndani ya uwanja huu wa maisha.

Itikadi za Waswahili wa mwambao wa Kenya ni pamoja na imani ya kuwepo pepo - majini, mashetani n.k; nguvu na uwezo wa pepo hao katika kulinda mashamba, mali, miji, kusaidia kutibu maradhi, na mashetani kuroga n.k. Itikadi hizi zina nafasi katika upwa wote wa Waswahili. Pamoja nazo, Waswahili wana mila kama vile ya miiko mbalimbali. Mifano: kula gizani ni kula na shetani. Kunywa maji msalani mtu huwa mwongo. Bundi akilia juu ya nyumba anatangaza kifo n.k. Mbaabu anamalizia sura hii ya mwisho wa kitabu chake na maneno haya: 'Itikadi ... zina mafunzo mengi yanayostahili kuhifadhiwa na kuzingatiwa '(uk.49).

Kazi kubwa ya kitaalamu juu ya utamaduni wa Kiswahili, ambayo tunaijua hadi sasa ni tasnifu ya udaktari wa falsafa iliyoandikwa na mwalimu Sengo² kuhusu Sanaajadiiya ya Visiwani. Mwandishi wake alivitalii visiwa vyta Pemba na Zanzibar kwa utafiti wa kina na kuibuka na hoja za kuueleza utamaduni wa Waswahili wa Visiwani kwa kuheshimu utata uliosababishwa na Bahari ya Hindi. Waswahili wenye wana michanganyiko, tangu ya maumbile, damu, historia, asili, sababu, matukio, itikadi, imani n.k. Bahari ya Hindi, historia ndefu ya Uislamu na lugha ya Kiswahili, ni baadhi ya sababu kuu za kuwafanya Waswahili kujihisi wamoja kilugha, kiutamaduni na kihisia. Uafrika asilia umepewa nafasi ya mwanzo katika haki na hadhi ya Waswahili. Suala la ugozi lisitazamwe kisiasa tu kwani kimaumbile watu tumepekwa rangi mbalimbali ili tutambuane na tuelewane kirahisi katika kuendesha mambo yetu ya kila siku maishani.

Ama mtafiti wetu huyu wa sanaajadiiya ya Visiwani amekiri katika aya yake ya mwisho tasnifuni kuwa kazi yake kubwa haikuwa kujaribu au kugeza kutoa jawabu za mwisho na za pekee kuhusu masuala ya utatanishi wa Bahari ya Hindi na Sanaajadiiya ya Kiswahili. Juhudi zake ziliishia katika kupendekeza hoja za

² T.S.Y.Sengo, *The Indian Ocean Complex and the Kiswahili folklore: The case of Zanzibarian Tale-Performance*. Unpublished Ph.D thesis. Khartoum University. 1985.

kurahisisha tafiti za baada yake zitakazolihusu eneo hili zito na tata la mwambao na ulimwengu wa hadithi-jadiiya za Pemba na Unguja.

Kazi nyingine ambazo zimefanywa kuhusu vipengele vyta utamaduni wa Kiswahili ni pamoja na *Tungo Zetu*³, kitabu pekee hadi sasa hivi ambacho kimezama kitaaluma na kitaalamu kuhusu Msingi wa Mashairi na Tungo nyinginezo. Mbali na mihemko binafsi ya uandishi kuhusu ugozi, Us wahili wa Was wahili na baadhi ya matukio ya Zanzibar ya 1964, Bwana Ibrahim Noor Shariff kajitahidi sana kueleza mapisi ya Was wahili na mambo yao. Kaweza kutufunza wengi juu ya urudhi yaani mipango ya tungo na kumkosoa Sheikh Kaluta Amri Abeid katika kitabu chake cha *Sheria za Kutunga Mashairi na Diwani ya Amri*⁴. Kuna mawimbi ya mihemuko dhidi ya juhudi za mwandishi K.A. Abeid lakini inarekebika bahari ya fikira za mhakiki inapotulizana katika kurasa za mbele. Ama sasa wasomaji wengi tunajua tarehe ya urudhi, utendakazi wa tungo, upungufu katika maelezo ya tungo na mijadala mbalimbali kuhusu kipengele cha ushairi, fani ambayo ina mapisi marefu sana katika Utamaduni wa Kiswahili. Kwa maneno yake mwenyewe, Bwana Shariff anakiri kuwa, "Iwapo ni kweli kwamba bahari ya tungo za Kiswahili ni ya maji makuu, basi ni wazi kabisa kuwa yaliyozungumzwa humu ni maelezo ya kimuhtasari tu kuhusu fasihi hiyo." (uk. 213).

Marehemu Shihabuddin Chiragh din hapaswi kusahaulika katika watenzi wa kazi bora za lugha ya Kiswahili na Utamaduni wake. Ama makala yake "Kiswahili na Wenyewe"⁵ yangelingana naye kwa hija, haja na jiha, uzito wake ungekuwa mkubwa zaidi. Hata hivyo, ye ye aliweza kujenga msingi madhubuti uliothibitisha kweli yakinifu kwamba Was wahili ni watu hai na hao ndio wenyenye lugha ya Kiswahili. Sisi wengine sote ni watumiaji na hatuna budi kurejea kwao - wawe na "vibandiko" vyao ama wasiwe navyo - kujifunza kutoka kwao na kujiimarisha katika utajiri wa Kiswahili asilia. Us wahili hivi leo si kinyang'anyiro tena.

Katika mlolongo mrefu wa waandishi wa kazi zetu, Maalim Hajji Chum amepewa fursa ya kutufungia dimba. Ama ye ye kashughulika sana na tafiti za lugha ya Kikae au Kimakunduchi na Utamaduni wake. Kwa watafiti wa Taasisi ya Kiswahili na lugha za Kigeni, Zanzibar, hayuko anayemkaribia kwa kuwa na data zake mwenyewe ambazo kajituma azipate ili aziandikie mabuku. Katika shairi lake la "UTAMADUNI UDUMU," Maalim Hajji Chum anatuwa idhi:

Kuna nyingi simulizi, ambazo zatia hamu
Za kale na siku hizi, kuzitunza ni muhimu
Tusiige upuuzi, ja kuabudu mizimu
Utamaduni udumu, vizazi hadi vizazi.

Mtafiti ameziendea mbio simulizi hizi na anazo za kutosha. Maandishi yake mengi yangeshakuwa vitabu hivi leo kama si wimbi la utatanishi katika mashirika ya

³ I.N. Shariff, *Tungo Zetu*. Trenton: The Red Sea Press, Inc. 1988.

⁴ K.A. Abeid, *Sheria za Kutunga Mashairi na Diwani ya Amri*. Dar es Salaam: East African Literature Bureau. 1965.

⁵ S. Chiragh din, "Kiswahili na Wenyewe". *Kiswahili* 44:1. 1990.

uchapishaji. Ama katika mswada huu tunaoufanyia kazi hivi sasa, Maalim Haji Chum anaeleza mapisi ya Wilaya ya kusini, asili za majina ya miji na mitaa, uchumi na mila, lugha ya Kikae, fani mbalimbali, ngoma, jando, daku, shomoo, miongo na sherehe za kuoga mwaka. Kazi hii ni ya msingi sana kwa mtafiti yeoyote wa Kikae na Utamaduni wa watu wa Wilaya yote ya kusini.

Umuhimu wa kazi hizi zilizotajwa na nyininge nydingi ambazo hazikutajwa (k.m. kazi za Mzee Hamisi Akida, Whiteley, Mnyampala na Shihabuddin, Mohamed Bakari, S.A. Muhammad, Mohamed Abdallah na kazi zote za fasihi) ni mkubwa sana. Tunatumai hivi karibuni tutapata kitabu au vitabu vitakavyojadili Historia ya Kiswahili kwa upana na undani wake, Utamaduni wa Kiswahili kwa kina cha haja na hivyo kuweza kukiegemeza Kiswahili Sanifu katika Kiswahili asilia ili kiwe na mashiko ya kudumu. Kadiri ya mapanuzi na maendeleo yake, makuzi na matumizi yake, Kiswahili Sanifu, kama lugha nyininge zote, sharti kiwe na kwao, kiwe na wasemaji hai wa kwenda kuulizwa kweli ya usahihi wa mambo.

1.0 ASSALAM ALEIKUM - ALEIKUM ASSALAM/CHEE-CHEE - CHEE-CHEE/SHIKAMOO - MARAHABA/AE

Baada ya kusalimiana, Mradi wetu wa pamoja, baina ya TUKI ya Dar es Salaam na Idara ya Masomo ya Kiasia na Kiafrika ya Helsinki, Finland, umeazimia kutafiti lugha na tamaduni za Kiswahili. Lugha na tamaduni hizi za kimsingi ndizo asili pekee ya kuhifadhi mapisi na maendeleo ya lugha yetu na utamaduni asilia wa Waswahili. Katika hatua hii ya mwanzo, kunatarajiwu kupatikana data zitakazowezesha tafiti-linganifu baina ya lahaja mbalimbali na kizaliwa cha lahaja hizo yaani Kiswahili Sanifu.

Ramani ya lahaja ikishachorwa na kuwekwa sawa, data za lahaja hizo na tamaduni, sanaajadiiya, fasihi n.k. zitahifadhiwa katika HIFADHI ya pamoja TUKI - Dar es Salaam na Helsinki. Makala na vitabu ni matunda yanayosubiriwa kwa hamu kubwa kuhusu kazi hii muhimu.

Mabwana Arvi Hurskainen na T.S.Y. Sengo wanamshukuru sana Maalim Haji Chum kwa msaada wake wa taarifa, tajiriba masikanini na ushirikiano wake mkubwa katika kazi ya utafiti uliofanyika Wilaya ya Kusini-Unguja yeye akiwa msaidizi wa kutegemewa sana. Moja ya sifa zake kuu ni wepesi katika unukuzi; kujitolea mhanga katika ukusanyaji wa data mbalimbali na kutokuchoka katika dhamiri yake ya kuuhuisha utamaduni wa wilaya yake na hasa wa Kae penyewe.

1.1 KARIBUNI TENA. KARIBUNI NDANI. NYUMBANI PENU HAPA. NAAM, TUPENI HABARI ZA UJAJI WENU.

Ama, makala haya yatajaribu, kwanza kueleza aina ya data iliyokusanywa; pili kudhihirisha utamaduni wa Kiswahili kwa kutumia data hiyo; na tatu, kuchambua

tanzu za utamaduni huo na kuonesha umuhimu wa mila na sanaajadiiya katika uimarishaji wa utamaduni wa jamii ya Waswahili wa Wilaya ya Kusini Unguja.

1.2 DATA ZA UTAFITI:

Kaseti ya kwanza imerekodi mazungumzo ya Bwana Mohamed Dume wa Kae, akieleza mkasa uliomkuta wa kuchukuliwa na maji baharini. Kuna mwensiwe aliyekimbia nyumbani kwenda kutoa taarifa:

- 1.2.1 "Yulya bwana akauka akaja zake Kae (Makunduchi ko) kuja lavya habari kuwa Dume kafu ama kaga... Haya hali ya bahari yevu mbaya sana... Hakulilawa kitu 'ta kimoja... Bahati yalya maji yakanleta tena juu kidogo kidogo kuno ko watu wamekuja Kae kusema kuwa nyifu..."

Haya hogolea hogolea mwenyewe bado na nguvu ambayo ni mambo ya miujiza mana sijogolea kiasi kikubwa ja siku hiyo...

Haya hogolea hogolea zaidi ya saa tano nyiwa kuko tu sijafika kukavu. Kwa bahati mawimbi yalya yakaja makubwa hwenda mbizi ili kuzuia yasinirushe vakubwa zaidi...

Haya hogolea kwa bahati nzuri Mwenyezi Mungu akanjalia kulya nnako kuchaka na maji yakawa yananveleka kuko. Kwa bahati hawa n'bahati henda mpaka vakavu...

Haya ikawa vua inakunya kunya, ngia ga uko kati hangia mlyia kati hakwa gunia hajifinika ili angalau nvate joto mana havana moto wakati no no tuwa chuvini...

Kwa bahati Mungu akanjalia ikawa silidhurika mpaka nkali hendelea na shughuli zangu za kuvua kama kawaida.

1.2.2. Mazungumzo ya jumla baina ya Mzee Mrisho Ali Vuai na Maalim Haji Chum.

MAV :Ee, miye jina lyangu Mrisho Ali Vuai

HC : Vano mahaa unavokaa vanakwitwa jaje, mwambie ga

MAV :Miwaleni ...

HC : Nawe tangu kuvyaligwa yako kuwa vano Miwaleni ama tena...

MAV :Eeeh, nyiwa vavava Miwaleni sijauka ...

Kaseti ya pili ina mazungumzo ya vijana wa skuli ya msingi Abdalla Ali Isa na Abdul Suleiman Haji. Nia ya kuyareekodi mazungumzo yao ni kuthibitisha uhai wa kikae, kwamba si lugha hai kwa watu wazima na wazee tu bali hata vijana wadogo na si wale wa majumbani tu bali hata walio maskulini.

Pia, Bwana Arvi Hurskainen anahojiana na Bwana Dume ambaye amekusanya mimea na kumtajia majina na baadhi ya kazi au matumizi ya mimea hiyo.

- 1.2.3. D: Uno Tuwi.
A: Uno Tuwi.
D: Ee, majani yake wanalya ng'ombe na mbuzi.
A: ...
D: Na mizizi yake vilya vilya tunatumia kama ni dawa.
A: Dawa ya?
D: Dawa ya tumbo na maumivu madogo madogo.

Kadhalika mna na paukwa inayotambwa na Bwana Hassan Ramadhani Abdallah kijana wa umri wa miaka ishirini na tano.

1.2.4 Paukwa - Pakawa

Aliondokea Makame wa Makame na mkewe ... wakavaa wana saba ... woti wanaume. Wakaja uwani, wakakaa kulya uwani wakamwambia baba na mama, tuna maneno kidogo, tunachaka tuchowee na nyuwe wazazi wetu. Aaa, tuna safari ambayo tunachaka kutenda ya kwenda soma somo kila mmoja analyochaka...

Kumbe walya wanakele wana nyota yao weka ya dunia tu iyo wayokuwa ni Mungu. Ikabidi siku iyo wakangia mlyia ndegeni na wakenenda kulya Ulaya, ... ikabidi wakaza masomo yao...

Wakasoma muda wa myaka saba iyoooo wakasoma, wakasoma, wakasoma, wakasoma. Hata wavyokwisa maliza masomo yao ikabidi sasa safari ya kurudi kwetu imefika. Wakangoja jidege lilya likaja valya wavofikia...

Kufika uko ikabidi wachukuu mabegi yao makubwa makubwa mna zawadi nyingi... Kufika kungia ndegeni ndege ikaza kuuka buuu safari kubwa kweli. Hata wakenenda karibu na nchi ya kwao kulya wakambiwa bwana mpaka sasa wezetu wanamwita pailoti haya suwe tunasema mwendeshaji wa ndege, wakamwambia ah, karibu vano njo venu...

Ikawa masomo yao kila mmoja watu saba kila mmoja na somo lyake...

... Yulya Mfalme akasema bwana miye shida zangu nyagiwa n'mwanangu Mariamu. Leo mwezi wa tatu sijamona na mwanaakele yenyuwe mwari. Mnavitambua?... Yulya mchawi ... mganga, ... akapiga bao akapiga bao, akapiga bao, akamwambia mfalme mwanaao kebwa ni jini. Na uyo jini kamchukuu kamveleka mbali sana...

Wajaza kuuka walya unju wakenda zao pwani wakangia mlyia mashuani walya wanakele woti saba wakenenda uko. Wakenda uko akofichwa mwana wa mafalme n' jini...

Mwizi yulya akawwa nguo zake nyingine akajitia chini chubwi baharini vubunuuu maji ya kanakwenda yulya mwivi... Akatenda kila rai akamwiba chwi...

...Sasa ikabidi majini wakaja zao juu kweli na yulya ayoja akamsuka naye akaja. Sasa wakaja wengi sana wakakaribia kilya chombo.

...Bunduki yani risasi zinawapiga majini...

Makame wa Makame akajengewa jumba ilyo kubwa sana ja lilya lya majezi yani ilyo lya gorofa lya juu kwa juu tena akajengewa akaishi uzuri kwa salama na imani na paukwa yangu ifikii yavo - po!

1.2.5 Baada ya kumalizika kwa paukwa hii kunatambwa nyengine na mwanakele (mwanang'hele) Muhamed Ali Jaku, msomaji wa darasa la nne, skuli ya Makunduchi. Umri wa miaka kumi wa mtambaji umeathiri fani ya paukwa hiyo. Maudhui yanahu haja ya kuzaa wana katika maisha ya ndoa. Ajabu ya haja hiyo kutokea katika siku kumi tu za maisha ya ndoa, baba akashindwa kusubiri. Mwana wa maua akapatikana unju, leo jioni kwa kesho. Mara mwana huyo akatumwa sigara, alipokataa kuosha vyombo, mamaake akavunja mwiko wa kumtamkia, NJO MANA KUWA MWANA WA MAUA. Akaruka!

Baada ya paukwa hii, kunafuata vitendawili vya Amina Mahmud wa Kipunguni Kae, umri miaka kumi na tano.

1.2.6.1 A: Mmoja mkali, mmoja mvivu, mmoja mtembezi

B: Moto, ipu (jivu), mosi (moshi)

Kaseti ya tatu ina maelezo ya Bi Sada Mjinga kuhusu mawaidha na mafundo ya maisha ya ndoa; siri ya jina Mjinga, vyungu vyake vine vya ndoa, kazi za wanawake wa Kae kugonga usumba n.k. Ama nia kubwa hapa ilikuwa kusikiliza Kikae katika uhalisia wake. Nayo ikatimu vizuri maana Bi Sada anakigomo sana Kikae.

Mzee Shaka Musa Ramadhani ni mmoja wa watambaji mabingwa wa paukwa. Hapa anashirikiana na Maalim Ramadhani Makame Ali Kishibo wote wa Makunduchi Kusini, kuisema lugha ya Kikae. Wazungumzaji wana maudhui yao ambayo si mepesi hufahamika kwa lengo la kudhihirisha ubobezi wa lugha yao.

Bwana Sigombe Maalim Isa anachowea Kikae cha Nganani-Makunduchi kwa lengo hilo hilo la wenziwe walio usoni kwake.

**1.2.7 SMI:Na kino Kikae kiasili ya miye haswa nnakuchowenza mana aswili
nvyaligwa Kae nkulii Kae mpaka sasa nyiwa ntu wa Kae. ...**

AH: Na Kikae kile ambacho unachowea sasa hivi ni Kikae cha wapi?

**SMI:Cha Nganani... Kwa watu wa Kae asili wa Nganani, walawii
Tumbatu. ... Mana mtu wa Kae, Nganani na mtu wa Tumbatu
akamchowenza kanavitambua, wanatambuana mpaka sasa wao waoko
wanatambuana.**

Maalim Seif anaendeleza mazungumzo na Bwana Arvi katika kaseti hii hii ya nne:

1.2.8 Mtu akafwa... maiti kemelazwa kitandani tunamsafisha tunamosa, tunatengeneza uzuri, tukesamtia ndani ya tusi tunamlavya nje hatunamtia kati ya tusi tunamtia ila bada kumosa na kumkafini. Tunamswalia tukesa mswalia tunamchukuu kumveleka uko madomboni. Akesa lavigwa kati ya usi tunamtia shimonii kwake. Ubao ulya tunamfunika ili ukati tunaoja mtia udongo ulya udongo usimkute.

Maalim Seif Makame Ameir anaendelea katika kaseti ya tano akielezea misimu na mengine mengi kuhusu embe, machungwa na faida za miti kama hiyo mjini Kae. Uchowezi huo unapanuka kwa hadithi zihusuzo uaghali na ugumu wa maisha kwa jumla. Baada ya hapo, tarehe 7 Septemba 1989, watafiti tulikwenda Paje na Bwana Arvi kupata fursa nyengine ya kumsikiliza Ayubu Haji Jecha pamoja na Mzee Ahmed.

1.2.9 Mzee Ahmed: Lakini kitu kimoja miye napinga.

Ayubu: Haya.

Mzee Ahmed: Kusema sasa ndo uzuri kuliko zamani. Pesa tele. Zile pesa tele haya haina manufaa.

Ayubu: Pesa haina manufaa.

Mzee Amhed: Ilikuwa shilingi moja ya Mngereza pishi nzima ya mchele, eeeh! Kweli, kweli. Ilikuwa ivo... Na ilikuwa mutukari mtu anapanda hapa kwa pesa salasini sumni apanda mutukari mpaka mjini.

Mnamo Septemba 7, 1989 watafiti tulifika Bwejuu na huko tukakutana na mtu mzima Mwarabu Khamis wa umri wa miaka sabini na mzee Ahmed Mgeni Tabu aliyekuwa na umri wa miaka mia moja na tano na akawa bado anaendelea kufanya kazi zake za umufti wa darasa za Dini pamoja na kutibia watu.

1.2.10 Ahmed: Basi miye... miye nyiyouka ku kale Bwejuu... na nlelegwa nyi Haji Ujinga, njo mume wa ovyo mamaangu. Mwalimu Sudi...tukenda tukasoma uko Uzini, tukenda tukasoma ninihii ilmu. Nataka kuyavya faida moja na watu wasikie waitambue. Ntapochuuzwa na mwezio watu wawili mkaendesha safi mnyoyo yenu Mungu kataingia akuongozeni, akawa mmoja mbaya kidogo basi Mungu atatoka mtie shetani akufisidini ja ivyo watu injewe wa duniani namna iyo.

Katika kaseti ya saba, Mwatima Ameir Haji anaanza na paukwa fupi juu ya maisha ya ndoa na tamaa za kupata mwana wa jinsi mke mwenye tende alivyomuachia tende hilo mumewe na kwenda kuolewa na mume wa pili. Maalim Haji Chum naye anatamba paukwa ya pili inayoanza na maudhui ya ndoa na tamaa ya kupata

watoto. Anapohojiwa na mtafiti juu ya umuhimu wa hadithi, Maalim Haji anasisitiza kuwa hukata tamaa mwanadamu ni kukufuru. Kisha wanajadili umuhimu wa uganga na nafasi ya kuweka dhamiri. Nadhari ni kitu cha msingi katika yote hayo.

Bwana Mohamed Abdalla (Dume) anatupa muhtasari wa maisha yake:

1.2.11 Jina lyangu Mohamed Abdalla (Dume). Nyalyaligwa Makunduchi, Nganani. Wazee wangu wote wa 'wa wa Nganani baba na mama. Nyalyaligwa 1946 na hakulia uko ko Nganani na shughuli zao mpaka hakuwa mkubwa, kiasi ya kuwa nde skuli henda hauelekwa skuli haza tangu darasa lya kwanza mpaka lya nane mwaka 1966 hamaliza. Maisha yangu kiukweli ya matatizo mana hatulija na msingi maalumu hasa wa kuwa tunajiendesha tunawa tunavo tu. Kivatiki ndivyo hakilivatika basi tunalala...

Baada ya kumaliza na Bwana Dume ambaye baadaye kajidhihirisha utu na ujuzi wake mwangi kwa watafiti, tukakutana na mzee wetu Bwana Mohamed Fatawi Isa. Mzee Mohamed anatoa mapisi ya aila yake. Wazee wake walitokea Bwejuu kuja Mfumbwi. Bwana Vuwa Kichachu akaiza binti yake Halima kwa mmoja wa hao wajaji. Bi Halima kazaa kina mzee Tuwani na wenziwe. Bwana Fatawi ni katika kizazi cha bi Halima. Mzee Fatawi akaiza binti ya Tuwani na watoto waliopatikana ni pamoja na Bwana Mohamed. Mama yao alizaa jumla ya watoto kumi na nne, Bwana Mohamed akiwa kifungua mimba.

Baada ya maelezo haya, paukwa zinifuata. Bi Amina Yusuf Hassan wa Nganani - Kae, alipouliwa ni Bwa Sengo kuhusu wapi ilikopatikana hadithi, Bi Amina:

1.2.12 Nyevu ntendewa n'bibi yangu kale wakati no nyiwa mdigi kuwa mtu ana imani mtu ana ahadi. Ukatua jambo ahadi niitengeneze nifise mji wa kuwa venu une imani mwezio kama shida umlanganizie nyevu utendewa vibidii yangu kevuakatwa mamie Kipengu.

Kijana Chamnda wa Skuli ya Kiongoni anatoa mchango wa mwimbo za paukwani.

1.2.13 Mke mdogo lamka tutwange
Twanga wewe uoukata mboribo wangu
Kubi, kubili!

Mke mdogo lamka tutwange
Twanga wewe uoukata mboribo wangu
Kubi, Kubili!

Mke mdogo lamka tutwange
Twanga wewe uoukata mboribo wangu.

Paukwa ya ubaya wa wanandugu waliomdhulumu mdogo wao wa saba inatambwa na kumalizika na waharifu kuuliwa kwa mzinga wakiwa melini na kwenye maji makuu. Dhuluma haifai.

Paukwa inayoifuatilia hii ni ya Amina Juma, binti wa miaka kumi na mbili. Vijana wadogo hukumbuka nyimbo zaidi kuliko maudhui ya paukwa. Baada ya hapa, tunakutana na Bi Mwanaisha Khatibu, mke wa mtu na mama wa watoto saba. Yeye anatupa nyimbo za kuchombezea wanakele:

1.2.14.1 M: Mwanangu Kidanga-diya kua nikupe wasiya

Mwanangu Kidanga-diya kua nikupe wasiya

Kuchunga kundilya mbuzi

Na ng'ombe unywe maziwa...

1.2.14.2 Usilie usilie mwanangu usilie '

Usilie usilie mwanangu usilie

Machozi yako yaweke

Siku ya haki ulie

Ujibwage bwage na chini

Watu wakushikilia.

1.2.14.3 Kilengelenge cha boga kutia nazi kunoga

Kilengelenge cha boga kutia nazi kunoga

Kilengelenge cha boga kutia nazi kunoga

Moyo watamani kula mkono hauna woga.

Bi Amina Juma wa darasa la sita, skuli ya Kiongoni-Kae na mkazi wa Kishangambuzi anatamba hadithi ya bwana aliyempata mke kwa mazingaombwe ya hirizi. Kitumishi cha Mfalme, kama ilivyo dasturi ya watu hao, kenda kumshawishi bwana wake aende kumchukua mke yule mzuri.

1.2.15.1 Tena wavyokwenda, tena wavyokwenda, akamwambia, aka akawa kanamfitini kanamwambia maneno tena yulya nani mke wa Makame wa Maka akadumba. Avyodumba, akamchukua.

Bwana kenda mbio kwa bibi kikongwe mtoa hirizi. Kamuelekeza ya kufanya. Akatumwa ndege kwenda kuimba juu ya kipaa cha nyumba ya Mfalme

1.2.15.2 Konko kororo konko

Kororo ntumwa n' Makame

Kororo ntumwa n' Makame

Kororo unke hirizi zake

Kororo unke vitu vyake

Kororo konko kororo konko kororo.

Siku ya saba, tena akalavya, bibi yule likageuka jijiti likenda na juu tu likapazwa likakatika na uwongo wangu wishi avo. Mamaangu. Maanake halinyambia.

Hadithi ya mwisho katika kaseti hii inahu ujinga wa mtu aliyepata siri ya kumfaa na jinsi alivyoitongoa siri hiyo kwa faida ya madhalimu. Dhuluma hiyo inasaidiwa na utamanifu wa Mfalme wa kutaka vyote. Mwishoni yulya mfalme naye akapigwa mikwaju! akapigwa mikwaju akapigwa mikwaju. Uwongo wangu wisi.

Kaseti inayofuata tunaye Mzee Shaka na paukwa yake maarufu ya Panjimaro, jitu kubwa lenye nguvu nyingi sana lakini mwoga sana. Kwa msaada wa mkewe, anashinda mitihani yote anayopewa na Mfalme ambayo kiundani ilikusudiwa imtie hatarini auliwe afile mbali. Hivyo aliweza kumgwia simba angali hai na kumpeleka kwa Mfalme kama farasi. Akaua joka na akapigana vita peke yake. Panjimaro anapewa ufalme. Na ujumbe wa paukwa hii ni kwamba mwanamke asidharauliwe.

Mzee Shaka anamalizia na kijimchezo kifupi kinachowababaisha Simba na Chui kwa hekima za kibalabala-sungura. Anachotaka kutilia mkazo mzee Shaka ni kwamba si mambo yote yatakayo maguvu. Mengi na ya maana yataka akili.

Nyimbo za msanja daima huwalenga wari harusi, bwana na bibi, kuwapa mafunzo yahusuyo maisha yao ya kila siku.

1.2.16.1: Muungwana bwana

Na mtwana bwana

Kipendacho moyo

1.2.16.2: Mwanangu mdogo kumono ushezani kafwana

Na asije kwao kashono upacho kavwaa.

Uganga wa shomoo ni maarufu katika miji ya Kusini-Unguja. Mzee Mgunya Mwinyi wa Kizimkazi anatupa maelezo mafupi:

1.2.17: S: Shomoo! Na shomoo ni kitu gani?

MM: Shomoo ni ngoma ya asili ya wazee... za mji, huwa unatengenezwa mji. La mji huwa unatengenezwa mji, huwa mji unatengenezwa mji huwa mji una vitu kama vibaya vilohusu ndo vinachomolewa vikatolewa vile vibaya ndani ya nchi.

S: Na hadi leo bado shughuli hizo zinafanywa?

MM: Ee, mpaka sasa tunazo:

Asema Kinole mwanangu Kinole
Kinole ufunue macho ulole
Mazali kuwa paka shume
Mlewa nyi watu tele

Kwetu asili yetu kusoma
Na kuagua mchanga
Tabatiyada abii lahabi-watabba
Uganga si wa bure
Uganga una masumbuo
Uganga kanyachii baba.
Baba haupigi chale mbili
Moja kimbelemele moja kituma nyongo...

Katika kaseti hii ya kumi, tuna maelezo ya kusaidia kufuta matusi wanaotukanwa Wamakunduchi. Ama Kihadimu si lugha ya watu wa Kae; nao kamwe si Wahadimu. Hivyo, ni Kikae, si Kihadimu, ndicho lahaja maarufu ya watu wa Kusini-Unguja.

1.2.18. Basi kwa hivyo mji huu ulikuwa unaitwa KAE kwa sababu watu mji ulikuwa kiombo kizuri kwa sababu maji yalikuwa karibu, kwa hivyo, wale watu wakaita, Kae hii. ...Sasa Seyyid wa Said tulipomwendea akasema, "tayari lakini fidia yangu mtanilipa nini?" "Tutakutumikia mpaka fidia yako itimie..." Sasa liko neno linakwitwa khadim ...ile khadim katika lugha ya Kiarabu ni mtumishi. Sasa yule Mwarabu basi pale ndipo akaweta wale Wakhadim manake Wakhadim watumishi. Ndipo ikaendelea kodi iyo wakamtumikia mpaka muda ukamalizika wote.

1.2.19: S: Je kuhusu msikiti wa Kichaka...?

HH: Msikiti-Kichaka stori yake.. watu wa Makunduchi wa kaskazi nausi, wanapanga mambo yao ya utamaduni ya uganga... Mwisho wao wanazunguka ulimwengu na Qurani yao wanasoma kama Khitima kuomba dua wakenda pale msikiti kichaka ndipo wanapoomaliza kuomba dua... Hiyo ndio khabari wanatumia ile mambo ya mila na utamaduni.

Mzee Mbaraka Mtobwe Ali wa umri wa miaka themanini na tano, akionekana na nguvu zake, kumbukumbu nzuri n.k; naye kapata fursa ya kutujuvya yake. Kapata kuoa wake wawili lakini hakujaaliwa kupata mtoto ye yeyote. Kuhusu tukio la kifo, maelezo hayapishani na yale ya kimsingi ya kumuosha, humkafini, kumswalia na kumzika. Nyongeza ya habari ni kuwa Kae, mavani kuna jina la pili na la tatu malaloni yaani makaburini. Kadhalika, kisomo cha tatu, chasomwa asubuhi na jioni. Vile vile:

1.2.20.1 MM: ... kwa hapa kwa kidasturi za ve petu hapa petu Makunduchi mtu akafiwa khasara yake ni kubwa kuliko huko kwa wenzetu... Maana hapa kila mmoja kanachukua chakula chake... kanachukua kila

kitu chake... akapika chakula chake. Ila siku ya takhatimu... lakini si peke yake pamoja na jamaa zake.

1..2.20.2 MMA: Watu wa Makunduchi si asili moja, wametokea sehemu nyingi.. Washirazi wapo hapa... Wagunya wapo hapa hapa...Wangoni wapo hapa hapa na kadhalika. Kuna Wazaramu wapo hapa hapa. Miye unavyoniona nna sehemu mbili... kwa baba yangu Mshirazi, nna sehemu kwa mama yangu ni ninihii Mzaramu... bibi yangu mzaa mama yangu kwao Bagamoyo, mahala huitwa Mnogotini miye sipajui... Na jina la bibi yangu Mwanate binti Kondo.

Kuhusu msikititi kichaka, mzee Mbaraka Mtobwe Ali alimshauri Bwana Sengo kwamba asiende humo msikitini ila kwa kupelekwa na mzale yaani muongozi maalumu. Kuhusu Kuoga Mwaka:

1.2.20.3 MMA: ...hicho ni kitu mustatiri... Huko nyuma usuli wake walivyokuja nayo siwezi kukwambia. Mana ala kuli hali mimi ni mkubwa si mdogo... hifadhi zetu imekuwa ni ndogo mengine hatuyalizi ila huyaona tu.

...Kabla Kukoga Mwaka tunayoyafanza. Maana kuondosha nukhs. Tunasoma Qurani, tahalili... Wassalaatullah Bashir, nadhiri tunafansa maana ni hijabu ya nchi yetu, tunafanza. Ilo ni lazima tena na mhanga ikiwa ng'ombe ikiwa mbuzi, ikiwa kuku tunafanza kila mwaka tunafanza.

- 1.2.21.1: Salama salama ya mjaliwa
 Muhindi na kunde
 salama salama ya mjaliwa
 Viazi na muhogo
 salama salama ya mjaliwa
 Tunaomba mji wetu
 salama salama ya mjaliwa
 Huyo ndiye salama
 salama salama ya mjaliwa
 Waeshi watoto wetu
 salama salama ya mjaliwa
 Mwende chuoni mtumwe
 salama salama ya mjaliwa
 Na sukulini mwende
 salama salama ya mjaliwa
 Msikize watoto wetu
 salama salama ya mjaliwa
 Msikilize wazee

salama salama ya mjaliwa
Tunaiomba salama
salama salama twenda zetu
Kwa heri kwa heri wee

- 1.2.21.2: Tambiko - Msikiti - Kichaka
Allahu Akbaru, Allahu Akbaru
Laa ilaaha illa llahu Wallahu Akbaru
Allahu Akbaru wa Lillahul Hamdu
Bismillahi Rahman Rahim
Wattini wazzaituni watturi siniin
Wa haadh Al baladi Al Amin
Ayatul kursiyyu...
Dua...
Nyiradi...
Qurani...
Khitimah...

Kusimama wima (hapo tena wengine wanapenya wenda zao); waitwa.

Kaseti Na. 12: Mtende - Kusini ya Kae. Nyimbo ya Mkwasa na Bi Mwaidi Nasoro

- 1.2.22.1: Kaka kinyogori wee poa moyo
Kaida ndiyo ilivyo we ya safari

TSYS: Umekwisha, haya ongeza nyingine. Hii ngoma ya Mkwasa inachezwa wapi?

MN: Sikwiji, sikwiji.

TSYS: Huwa inachezwa wakati gani, kwa shughuli gani?

MN: Miye nyijua mwida tu.

Bi Sada biti Nyinga wa Makunduchi - Mzurikaja na wensiwe kina Bugani, Amina Haji, Amina Ame, Mariam Ali, wana nyimbo za Msanja. Kabla ya nyimbo hizo, Bi Sada ana maelezo:

- 1.2.22.2: Mwanamume mwanamke akafundwa...maana hii ngoma siye tuikutu hapahapa...

Latifa Datu wa Mkadini - Kae na wa skuli ya Kiongoni, anatamba paukwa ya Kaka na Dada katika kaseti yetu nambari kumi na tatu. Ama Ali na Fatuma waliambiwa na baba yao, alipokuwa mahututi:

1.2.23: Miye wanangu nakufwa heya na vitu viwili, kifa mtu achague anachochaka. Na radhi na mali, mnachaka nini? Yulya Fatuma akasema, miye nachaka radhi, na yulya Ali akasema, miye nachaka mali.

Mama yao pia, alipokaribia kufa, aliwaliza swali hilo hilo. Kila mmoja akachagua kile kile alichochagua kwa baba yao.

Ali akaoa, akazaa. Mali yake yote ikamwishia. Hata siku moja, Ali alikwenda kwa dadaake kuomba maboga. Alipoambiwa hakukuwa na mapevu bali machanga tu, Ali aliamua kumuhasiri nduguye kwa kumkata mkono. Fatuma akahama na kutokomea porini. Akalala juu ya mti usiku mmoja. Chini yake palikuja asikari. Asubuhi wakachukuzana hadi nyumbani kwa mwanamume wakaishi pamoja bila ya ndoa halali. Bibiye akajifunga na kujifungua. Baba mkwe wake alipogundua ukwe asiouja, ikabidi Fatuma asumke. Njiani anakutana na joka, linamtaka msaada, analipa. Wanafuatana hadi chini ya bahari. Siku za kuondoka, Fatuma anapewa 'kipete-wa-kipete'. Akakisuga kipete akapata jumba kubwa. Akawamo ye ye na mwanawewe. Kakie Ali kampitia pale siku moja kumuomba mkate. Bi mdogo kakataa kutoa mkate na hata udugu hakuutaka akikumbusha jinsi alivyohasiriwa mkono wake. Mtambaji anasisitiza thamani ya radhi, iwe ya wazazi au ya walimu.

Paukwa ya Shida Pandu Kinange inahusu mwiko wa kuapa. Mke anaambiwa na mumewe, 'kwetu hukugomo we mana hakuna lapwa', ye ye anadai lazima waende. Walipofika:

- 1.2.24: Mke yangu nikwambii
Mimi kwetu hakulapwi
Nawe sasa umelapa
Tena kuapa Wallahi
Mzee Mkondo njo ulole mambo
Mzee Mkondo njo ulole mambo!

Mwanamke kaponea chupuchupu kuliwa na mazimwi.

Paukwa za kina Chaunda Mazi, Mohd Fadhili, Semeni Khamisi, Qaima Omar, Fatuma Asani Selemani, Abdalla Ali Isa, Mabruki Mhamed, Hadiya Saidi Amuri, Yasia Hassan Muhammad, Sharifa Kinole Musa, Mwanakombo Ameir, Amri Mohd Haji, na Maryam Nasor Suleiman, wote wakiwa wanafunzi wa skuli ya Kiongoni, ndizo zinazofuatia baada ya hapa. Maudhui makubwa ya paukwa zino ni masuala ya ndoa, haja ya kuzaa, jitihada za kuombea watoto, malezi ya wake wenza na watoto wa kambo. Mfano, paukwa ya Maryam inafunza mama wa kambo wasiwe wabaya kwa watoto wao wa kambo.

Uswahilini kunafahamika sana kwa itikadi za kuwako kwa majini. Bwana Muhammed Abdalla Dume, mume wa wake watatu na baba wa watoto kumi na tatu, anatueleza kisa kimojawapo ya visa vingi vya mji na viwambo vyake.

1.2.25: ... Akenenda, akenenda, akenenda, akanenda mpaka avyofika Saateni valya vanavo mafulio vo vana watu wanafulia nguo na madobi wakubwa wakubwa...akamkuta mwanamke mzuri kweli kweli kwa sura mana

kananukia...ehe! yuno mwanamke yuno kwa miye barabara yu...ujana umshiki kila mwanamke kamkaza kwa yeze tu... yuno kamba njo yuno mana hanatosheka na mmoja...sasa yulya bwana akona aah! yuno mwanamke mbona hamba hanantia wasiwasi, hanantazama kajifiniki tu. Yalya macho yake akamlola ga miguu...mbona hamba ina makwato...nyusi hana wala kope. Ah, yuno mtu jaje...meno yawa javilya jembe ja lino jembe...yuno si mtu, miguu ina makwato ya punda... Miye nsumke, nyisumke ...kanalola nyuma akono yulya sasa nyimgomu nyimsumku...

Akenenda hana wasiwasi tena avyofika valya wakadawiana je salama - salama. Habari za wapi? Ah, nalawia uko...Akawambia, nalawa Saata nalawa mtoni kwa msichana wangu, sasa nvyokona nrudi hona nrudi miye ili nyangasie kazini...Halafu hamkuta mwanamke njiani naye hamtongoza, kumtongoza akadumba...nyvolola miguuni kana makwato ya punda...

Sasa walya watu watatu wopya wakenua miguu yao: iyo miguu iyo ja ino? Mmh! yulya mtu akagwa vano tena haliuka...kazini njo halikwenda ye kagu vano valya...unju...watu wanavita...twendeni tukamlamseni...askari...wakaja, akashitukwa shitukwa kumbe mzima njo kagu kwa woga tu.

Mpaka leo kijana uyo kakomo kwa kumkuta mwanamke akamtongoza katendeke kasilimu mswaliji ja vyo hako.

Bwana Dume anatupa habari za mkasa mwingine.

1.2.26: Wakati wa siasa kuno kwetu kwevu na vituko mbalimbali watu wavyoja wakatendeana...bwana kuna mkutano siku kadha Nungwi na mnahutubia mzee Karume...Na yulya Nura Mhindi na Wahindi hawalijawa tabaka moja na suwe watu weusi, kana uhindi wakwe tu mbali...Wakangoja gari safari yevu kiasi saa 9, mkutano uwe saa 9 Nungwi, safari iwe kiasi mnamo saa 6 vino wauke Kae wende na Nungwi. Wakakaa watu wao gari hainalawa, haijaja...Yulya bwana akauka akenda avyofika kwa Nura kanakona ilya gari iwavo heya haina dereva. Jaje bwana we suwe tunachaka kwenenda...Ah, gari mbovu. Kanatenda ja vilya makusudi ili walya watu wasende mkutanoni hali gari yo zima heya yake...kaseme gari mbovu.

...Kamati yo ya tawi Watu kumi na wawili wano wakapanga jama njo kweli suwe mkutanoni tusende Nungwi, wakati mnakwenda kuhutubia yeze mzee. Vigumu, tena sasa tutende jaje na hatuna chombo!

Akamka mzee Maliki, Ngojani ga miye nde kuno nyumbani, naweza kwenda kutambua mashauri ya kutenda. Valya akabaki Pecha, akabaki Hajji Jecha, ba Msa Juha...na kina mzee Ali Kikuni jumla yao watu kumi na mmoja...Ta, tumngojene ga yulya mwenzetu huwa akaja na mipango mipy. Kumbe yulya bwana avyouka valya...kenenda mpaka kwake...vana mtungi una maji mkubwa kiasi uno mtungi wa kungia debe kumi na mbili...nka ga no mtungi, kanamwambia mkewe. Mtungi una maji. Heyamimina umo dooni...akachukua mtungi ulya akalola viwambazani vano akona kawa ja hino lya kufinikia vyakulya, nyambwe nyambwe. Akaja zake mpaka mharitani njiani weziwe wanamona...Hawawiji ulya mtungi una maana gani...

Akafika mpaka walipo, akatua mtungi, kawa liwa mkononi. Haya sasa, akawambia, `safari iwako' Safari iwako? Eeh! kuvata gari gani? Gari ino. Uo

mtungi? Eeeh. Sema yano yachawa mambo. Je, nuwa tayari tuchakwenda? Akasema wengine, `Suwe mtungini hatungii. Hamngii jaje? Mba mtungi haunangia mtu! Akambia, Basi, kama mtungi mtu kachagoma kungia, ngia ga wewe uko kati ya mtungi. Ukangia naswi tuchangia. Eh tuchangia. Mchangia? Eh.

Haya changia munlole. Akangia kati ya mtungi. Akenua ga mguu akatia kati ya mtungi akenua na wa pili akatia mtungini, akakaa kitako hawana mona...halafu akalawa, mnyono? Tukono. Mnyono? Tukono.

Sasa na angie mmoja baada mwengine. Akangia ba Msa Juha, akangia Haji Jecha, akangia Pech na Ali Pira Shor wakati uo njo cheyameni wao eeh watu woti kumi na mmoja wakangia akabaki yeche na kawa lyake mkononi. sasa nami nangia.

...Si watu wa kale tu njo watu wakongwe wakongwe mana Kamati yevu na watu wakongwe watupu hamna kijana. Yulya bwana akalichukua kawa lyake nyangwe nyangwe akalifinika kuno juu ya mtungi halafu akawambia sasa tunakwenda. Akaupiga ndofya (kuupiga kwa kidole) ulya mtungi ukatoka. Unkenendaa, unkenendaa umo umo kati ya mtungi wanazungumza hamba wawa garini wanatikatika vijichwa tu mpaka karibu na Nungwi, vana uwanja, mtungi ukaja zake chini...akafunua kawa lyake yulya bwana akalawa mmoja mmoja, watu wanasingaa wano watu wanawalia mtungini wanawalia wapi wa?

...Wakenda kwa mzee Karume valya wakadawiana watu wa Nganani `Ndo nyie watu wa Nganani mmekuja? Eey tuja. Sasa suwe tunarudi bwana mkubwa, tuja mkutanoni tu. Heya gari yevu itukorofishi hailikuja gari. `Tena mja kwa nini?' Tuja kwa mtungi bwana. Mtumii maarifa gani? Ah maarifa tunayo swiswi...walya bwana wakarudi wakajitia mtungini mwao wakaja zao mpaka wavoukia.

TSYS; Na mzee Maliki yupo karibu hapa?

DUME: Mzee Maliki kawa karibu

TSYS: Mambo yake bado anayo?

DUME: Aa, kanayo haja hajacha mambo ayo

Kaseti inaendelea na paukwa ya Yasini Asani Mhamadi ambayo inatuelekeza tusidharau wanyonge yaani tuwaheshimu watu wasiokuwa na fedha kwani fedha ni maua, leo yamechanua kwa huyu, yakinyauka, kesho kuchanua kwa mwengine.

Simini Khamisi Yusuf anaimba mwida wake kuhusu `Mapenzi maua popoti huchanua' na kutuhimiza tukalijenge taifa. Adira Mohamedi anaimba mwida wa Sikweli. Kadhalika Fatuma Asami Selemani:

1.2.27.1: Baba na mama msinkatize
kwenda shulenii kusoma
Elimu ya sasa ishaniongoza
niache nisimulie

1.2.27.2: Sharifa Kinole Musa:
Baba mtoto simuoze mume
Ngoja kwanza amalize shule

1.2.27.3: Sinuni Khamisi Yusuf:
Maneno myochoweya yo,
myachowee kwa vyema
Makuti yanapepea yo,
Makoroma chendasema

Mhamed Majoko ana hadithi yake nzuri kuhusu itikadi ya vibwengo na jinsi wanvyomisaidia bwana mmoja masikini baada ya huyo mtu kumshinda kibwengo kwa fimbo na aya za Quran. Mtaani watu wanasituka kwa choyo na inda. Hadi anatokea nduguye wa damu kwenda kumwuza viwaje ala vyakula vya samli. Bwana Sheikh anamfahamisha na hata kumchukua pwani. Huyo nduguye katoka manusurani kuuliwa na kibwengo kama si kwa msaada wa kakaake.

1.2.28: ...Yulya bwana ikamjia roho ya tamaa yulya ndugu mwawa haviji kusoma. Akauka akenda weka na mishipi yake mwenyuwe akenda akavua samaki valya mara kanasikia, `Weye bwana we. We kunaharibu samaki wetu bwana kuja tafuta nini?' ...Nyulta hamna samaki sijui...Fimbo zimekugwa, ye kusoma haviji masikini! Alitandikwa fimbo ... miti inamgwa ...miti inakugwa tu.

Sasa yulya ndugu mtu kanalawa msikitini akavita kwa ndugu yake akauza, 'Fulani kawa wapi?' Vano kauku kachukuu mishipi kende pwani. Allah Akbar -- kakaamtu kenda mbio kumuokoa.

Kakaamtu kenda mbio kumuokoa nduguye ambaye alisumbuliwa sana na inda ya roho, choyo cha moyo na uhaba wa fikira. Ndipo Waswahili wakanena, 'tamaa nyangi mbele kiza'.

Katika kaseti yetu ya kumi na tano, tunakutana na baadhi ya vijana wanaoanza kuuliza maswali ama kurekebisha itikadi ya mizimu ambayo imeshika sana katika tamaduni za viambo vya kusini. Shauri Ali Shauri, wa darasa 10B, skuli ya Jambiani, anatueleza tajiriba ya mzimuni alikokwenda kitambo cha siku za kuhesabu kabla ya kufika kwetu:

1.2.29: Avo nyuma si chini ya wiki tatu twevu twende mzimuni unakwitwa Kuumbi. Lakini miye silikwenda mizimu, nyevu nyendee nkapige mchele tu halafu nrudi. (vicheko)...

Sasa bada kufika tu valya wakaza kuomba, 'kwa niaba ya mizimu sijui na wazee wa mzee Mkazirondo tunaomba mizimu wetu utupunguzie matatizo'. Bada avo nkakikuta kilya nchokusudia tukapiga mchele (vicheko)

TSYS: Huo mizimu ni mizimu wenu wa jadi?

SAS: Eee.

TSYS: Sasa kwa nini wewe umefuata mchele tu?

SAS: Kwa sababu wanakosea katika zilya harakati za kuomba - katika harakati za kuomba wao wakaomba wao wanasesma, 'Mizimu weye tunakuomba'. Sasa jambo linalyontenda nsishiriki kuwa hawana mtaja Mwenyezi

Mungu wanataja mzimu - tunamuomba mzimu uno kadha kadha sasa yalya njo yayontenda nsishiriki.

TSYS: Nao ni Waislamu pia wazee wako?

SAS: Eee.

TSYS: Lakini wamesahau Bismillahi, siyo?

Mariamu Haji, darasa la nane, skuli ya Paje Ostabee, anatoa hadisi ya Makame wa Makame aliywewa Mboja ambaye ni mke zimwi.

1.2.30: He! jamani miye nyiwa mzuri kila nnakaa najona nyiwa mzuri heya uno mkia unannanga bora nyiukate. Akatua mkia wake chini ya mti akachukua jijibwe akaa kanakwimba:

Ewe mkia dumka wee

Mayongwe

Ewe mkia dumka wee

Mayongwe

He! heya yuno Mboja kila siku kanatendaje uko? Akaa kanakwitwa, Mboja Mboja, akaitika akasema, `Ngojani nakuja ... alipokuja hana kuni. ... We kila siku kunangia...uko kwenda ukatendaje siye tunageza kunapata kuni kweli uko ... Miye nkwambiini kwetu silizoea kwenda kunini miye sinazipata...

Washiki kumchungia wakasema, mnakona Makame wa Makame tumwambii yulya mkewe zyimwi heya kashiki si zyimwi. Basi tukenda tukamwambieni... Tena siku ya beni ukatiwa ule mwida uowowo ... watu wanakwimba: `Ewe mkia dumka wee Mayongwe!'

... na yule yule Mboja mke ya Makame wa Makame kashiki uwanjani watu telee njo wa harusini wa benini, kashiki katoa jikia lake kanaligaragiza lijaa madondo (vicheko) wakakaa watu wanacheka.

Yulya Makame wa Makame akambiwa, `kwambiwa zamani mkeo zyimwi, umwache, we kushiki si zyimwi, kunakona sasa kesha kuonesha uzyimwi wake nawe kunakaidi tu'...

Mwatima Abdul-Fatahi Musa wa darasa la nane, skuli ya Paje, anatamba hadithi ya Ng'ombe na Punda. Anayefuata ni Badru Abdalla wa darasa la sita, skuli hiyo hiyo ya Paje na kuishi Paje-Shafaki, anatamba hadithi ya kima ambayo, tafauti na wenziwe, ye ye hii yake kaisikia katika kipindi cha watoto redioni.

Msanja wa Paje

1.2.31. MH: Babu Kombo nja kwako
nkwambie yangu ya mdomo
Uniozeshe kikongwe
mana chekibobu simgommo.

Ameir Nishadi wa Jambiani Miuli, darasa la 10B skuli ya Jambiani anatongoa hadithi ya wanyama waliomuhamakia mwenzao sungura - kwa kukataa kuchimba nao kisima na kisha kwa kuwatibulia maji yao. Siku moja wakamgwia na kumtatiza kamba ili wamtose. Kalia, kaja mtaminifu mmoja akataka afungwe yeche ili amwoe binti Mfalme kama alivyodanganywa na sungura. Wanyama waliamua kutekeleza maamuzi yao ya kumtosa yule mtu mradi ndiye aliyekutwa katika tatizi zao. Baada ya muda wa miaka kupita:

1.2.32: Sungura akajiawiza shimonii mwake kavwaa koti zuri na kanzu nzuri na kofia yake ya viua. Sasa kwa bahati akakutwa nyi mzee Bweha, Je, mzee Sungura viyi ulikuwa wapi? ... Miye bwana nyevu nde peponi, peponi kuzuri sana. Binafsi kunavyona nvyovwa nguo zangu zino na nvyofana! Akasema, Eee, nokona. Lo tupeleke naswi. Haya, ngojani chakupelekani. ... wanyama wakubwa wakubwa wakesa ikabidi kabaki weka.

Zimamie Usufu wa Jambiani Kibigija, darasa la kumi na moja miaka kumi na tisa, skuli ya Jambiani anatoa paukwa yake inayomuhusu Makame wa Makame na ndoa yake, na wanawe Ali na Mosa. Dhamira kuu ya hadithi ni wivu, inda na dhoyo cha mama wa kambo dhidi ya watoto wa mumewe.

Vitendawili

1.2.33.1: Idirisa Haji Tabu - kikadini, Fomu III. Skuli ya Jambiani
-- Prrr mpaka Makka

: Saida Abdalla Mwinyi, Fomu IIA, Skuli ya Jambiani
-- Utelezi

1.2.33.2: Saida Abdalla Mwinyi
-- Shata shiti fedha jini wal-bahri
: Sharifa Ali Suleiman, Fomu III, Skuli ya Jambiani
-- Nazi

Vitendawili hivi winadhihirisha na kuthibitisha Uswahili ulivyo utamaduni wa Kipwani - bahari - majini na minazi, kadhalika Kiislamu - kwa mwendo wa utelezi, mtu akafika Makka kwenda kuhiji kwa mbio za ajabu kama mtu apigwapo mwereka na utelezi. Kijana Idi Asami Haji wa Fomu IIA Jambiani anatamba paukwa ya Paka na Korongo inayozingatia wasia wa kutotendeana ujanja - utapeli, uhuni n.k. katika maisha. Mwisho wa kaseti yetu hii muna maelezo yahusuyo itikadi ama jadi ya mzimu. Kijana Ameri Nishadi wa fomu IIB Jambiani Miuli anajibu maswali ya mtafiti

1.2.34: TSYS: Hayo mambo wewe umewahi kushiriki?

AN: Nvyojawa mdogo nyevu nkashiriki. Heya sasa sinashiriki

- TSYS: ...Na wanapoomba wanamuomba nani Mungu au wanaomba vitu vingine?
- AN: Humwomba Mungu na valya makaa wanavokwenda
- TSYS: Wana itikadi napo kwamba wakiomba pale wanapata mahitajio!
- AN: Wanapata! Ja wana kwenda wakomba na mambo mengine tu
- TSYS: Sasa kwa nini wewe hushiriki?
- AN: Kwa sababu miye nakona kamba hayana uelekeo na miye kwa akili yangu inavyonka
- TSYS: Huyaamini tena?
- AN: Miye ta (vicheko) siliyaamini
- TSYS: Ahsante sana.

2.0 TUNAKUSHUKURUNI KWA TAARIFA NZURI INAYOHUSU UJAJI WENU. KAMA MJUAVYO, HAPANA ZIADA MBAYA. TUPENI KIINI CHA MAMBO YENU.

Kazi kubwa ya sehemu hii ni kuonesha, kudhihirisha na baadhi ya mwahala kuthibitisha madokezo na mapendekezo yahusuyo mapisi na utamaduni wa Kiswahili kama yalivyojitokeza katika data hai ya masikani hai ya Kae, Kizimkazi, Mtende, Jambiani, Paje na viambo vidogo vidogo vya Kusini-Unguja.

2.1 WAMAKUNDUCHI

Wamakunduchi ni Waafrika weusi wa Wilaya ya Kusini-Unguja. Ni watu wanaotosheleza sifa zote za umwambao kwani wamo ndani ya Kisiwa kimojawapo kilichopo pwani ya Afrika Mashariki. Watu hawa na majirani zao wa wilayani mwao, wanaonekana kuumili uafrika katika majumbo yao, majenzi yao, makulaji yao, namna zao na lafidhi za lugha yao ya Kikae ambayo sisi watafiti tumeionna kuitawala wilaya hiyo nzima, kama ni tafauti za Jambiani, Paje, Kizimkazi, Muyuni na Kae kwenyewe, ni ndogo ndogo sana. Ni watu wa asili ya Kiafrika ambaa hivi leo Afrika nzima ina kila sababu ya kuwajivunia kwa hadhi yao ya kuwa mionganoni mwa wazungumzaji lugha (lahaja) mojawapo ya Kiswahili.

Dhahiri ya uyakinifu huu, anaitoa mzee Mbaraka Mtobwe Ali katika data Na. 1.2.20.1 anapotaja Ugunyani, Ungonini, Uzaramuni hadi kupataja Mngotini Bagamoyo na kukumbuka jina la nyanyaake Mwanate binti Kondo kwa Jumbe Mtoro kuwa ndiko kwao yeye kwa asili yao. Ushahidi zaidi ya huu umo katika lugha na utamaduni wao. Lau wangekuwa wana dalili za ujio wa kigeni kama wachache wao wanavyotaka kujinasibisha na Ushirazi wa Irani ya leo, kungeonekana "vitu vya asili na majina ya kigeni na mengi yenye kufanana na lugha nyingine"⁶, kama asemavyo Mzee Hamisi Akida na kuungwa mkono na data

⁶ Mzee Hamisi Akida, "Utamaduni, matumizi na misingi ya lugha ya Kiswahili", **MULIKA** 11, 1977. Uk. wa 10.

za kitaaluma za kina Graham Connah na Nurse na Spear⁷ na kudondolewa kwa haja kama hii katika makala yangu ya *Waswahili Customs*.

2.1.1 Utamaduni

Utamaduni wa Wamakunduchi ni hai katika hali zote. Taarifa ya kufa au kupotea kwa Bwana Dume, data Na. 1.2.1 ni ushahidi wa utamaduni hai wa baharini. Kuna tafauti kubwa baina ya kupotelea baharini na msituni. Itikadi ya vibwengo inayoelezwa katika data 1.2.28 ni ithibati ya utamaduni wa kibahari na kipwanipwani. Hadithi na simulizi za kukutana na majini wa kike kama ilivyo katika data Na. 1.2.25 ni ithibati ya sanaajadiiya ya Waswahili.

Safari ya kuruka na mtungi, data Na. 1.2.26 na paukwa za kitekinolojia data Na. 1.2.4 ni mambo mawili yanayodhihirisha kweli tata ambayo ni ngumu mno kuikanusha na nzito kuingia akilini. Itikadi hizi zilitiwa katika chunguni kimoja na taarifa za kukoga mwaka data Na. 1.2.20.3 na uganga wa hirizi data Na. 1.2.15.2 na mila za kupa watu majina yenye maana k.v. Mjinga, Mgunya, Mwinyi, Kombo, Mtobwe nk. uafrika unajidhihirisha wenyewe bila hata kutafutwa.

Tambiko za Mswahili zimemili zaidi katika Uislamu kama watu wa Kae wanavyoudhihirisha mzimu wao ambao hawauiti tena mzimu bali msikiti-kichaka. Kama data Na. 1.2.21.2 inavyoonesha, ni Allah na Qurani yake, ndivyo vilivyotawala. Hata hivyo, mwacha asili mchawi. Nadharia ya sanaajadiiya inayosema jadi haifi kwa urahisi, inajieleza yenyewe katika tambiko za kijadi zaidi za siku za ujahiliya ambazo ng'ambu tu wilayani Bagamoyo na Kisarawe bado zinaishi na baadhi ya majirani k.v. baadhi ya Wakwere na Wazaramu ambao bado wanashikilia itikadi za wazee wao kina M'hengo na Sagara, kina Pazi n.k. Data Na. 1.2.29 inayotaja kuombwa mzimu wa wazee wa mzee Mkazirondo na data 1.2.35 inavyoonesha shiriki ya kumwomba Mungu na papo hapo kuuomba mzimu kunadhihirisha mapisi ya asilia kabisa ya uafrika wa Mswahili na jinsi dhana ya shiriki ya Mwislamu Mswahili ilivyo tafauti na ile ya wengue.

Mila ya kuolewa ili kupata maisha ya heshima ina uzito wa kipekee Uswahilini. Binti mdogo wa Ki-Kae yu radhi aolewe na kikongwe kwa haja ya kupata heshima yake katika jamii kulikoni kuolewa na kijana ambaye kwa Kiswahili cha ujana anaitwa chekibobu. Data Na. 1.2.32 inathibitisha hali hii halisi ya tabia mbaya za hao machekebobu.

Taasisi ya Msanja imechukua nafasi ya ile ya Unyago na jando. Wilaya ya Kusini yote imejaa ngoma za msanja data 1.2.22, 1.2.32, 1.2.27 n.k. kwa minajili ya kukuzia, kufundia na kufunzia vijana wao ili kuwa na jamii inayokubalika kitabia. Nayo hii, ni taasisi inayothibitisha upekee wa utamaduni wa jamii hii ya Wamakunduchi, Wajambiani, Wapaje na Watu wa Wilaya ya Kusini Unguja kwa jumla.

⁷ Graham Connah, *African Civilization: Pre-colonial cities and states in tropical Africa. An archaeological perspective*. Cambridge. 1987. Uk. wa 151. Pia Nurse na Spear, *The Swahili*. Philadelphia. 1985. uk. wa viii: "Waswahili ni Waafrika waliozaliwa na kukuzwa barani Afrika..." (tafsiri yangu).

Hapana shaka, matanga ya kusoma tatu asubuhi na jioni na hasa ushirikiano wa kila mtu anayeshiriki matangani kubeba, kupika na kula kiliwa au kilaji chake mwenyewe data 1.2.20 ni mila ya kipekee kabisa katika mila za pwani ya Waswahili. Haijambo hii ya tatu kwani ina usuli katika mila ama dasturi za Waislamu. Lakini tabia ya kwenda na chakula cha kula kila mwendaji matangani, hii ni yao peke yao hadi hapo tutakapowapata wenzi wao.

2.1.2 Kikae

Kikae na vilugha vyake vinavyosemwa Mtende, Kizimkazi, Jambiani, Paje, Mvyni n.k. ni lugha ya pekee katika lahaja za Kiswahili. Upekee wake uko katika uhai wa lugha hiyo kwamba katika skuli za kusini lugha inayotumika ni hiyo pamoja na kuwa walimu na wanafunzi wanao uwezo wa kuchowea kwa kisanifu pia. Watoto wadogo kwa watu wazima na wazee yaani tangu vinying'nya, vitukuu, wajukuu hadi wana kwa nyanya na babu zao, hapana lugha ya maana ya kuitambulisha jamii yao ila Kikae. Ama tambo za paukwa zitambwazo na wanakele ni ushahidi tosha wa uhai wa sanaajadiiya, fasihi simulizi na lugha yenye ya Kikae katika wilaya ya Kusini, Kisiwani Unguja.

Kuna maneno kadhaa niyajuayo kuwa yanafanana na lugha za ujiranini katika ukanda wa pwani ya Afrika Mashariki. Neno *kuuka* liko katika Kikae, na kwa maana hiyo hiyo ya *kwenda*, *kuondoka* n.k. limo pia katika Kimakonde na Kiluguru. Kae ni mji katika Kikwere, *kaya* ni Kizigua kwa maana hiyo hiyo. *kulavya* kwa Kikwere ni *kulava* kwa maana hiyo hiyo ya kutoa, na *kulawa* ni *kulawa* kwa Kizaramo, Kikwere na Kizigua kwa maana ya *kutoka*. *Mwenyuwe*, *nyuwe*, *suwe* ni Kizigua nje ndani kwa maana hizo hizo za *mwenyewe*, *nyinyi*, na *sisi*. *Nyagiwa* huenda limechimbuka Ukwereni ambako ni *nyagilwa* (kutokana na *kwaga* = kupotea) kwa maana ya *nimepotolewa*. Senteni kama hii... *ayoya akasumka* tunaweza tukazihusisha na Kiswahili cha kanda ya Mtwara k.m. ...*misitu minene walimokiishi daima*.⁸

Maneno kama *madombo* kwa maana ya *malalo*, *mava*, makaburi yanazidi kuturudisha katika uasili wa Kiswahili kabla ya kuongezewa kaburi kama lilivyo *mapisi* kutoka pwani ya Kenya na kabla ya kupewa tarikhi na *historia* hata yakashika na kututia uvivu na sahau kwamba tuna chemchem za Kiswahili ambazo bado hatujazichota, zenye wingi wa maji matamu na ya tunu kwa lugha yetu. Ama leo tumeanza tu kuzitalii lahaja za Kiswahili na kupata maneno kama *hazigi* lililofichwa kwa muda mrefu na maneno *tabibu* na *daktari* wa madawa. Yatosha hadi hapa kusema kuwa lugha ya Kihadimu haipo. Hakuna lugha inayowanyanyasa wenye lugha. Kihadimu ni "kisaidizi" au lugha ya "watumishi/wasadizi". Mapisi ya uonevu na unyanyasaji yamepita. Lugha ya wilaya ya Kusini ni Kikae. Data Na. 1.2.18 inatuthibitishia ukweli wa kimapisi.

⁸ P.E. Ladda (Mhar.), *Mchango wa Mtwara katika ukombozi Tanzania. Mkoa wa Mtwara*. 1982. Uk. wa 10.

2.1.3 Sanaajadiiya ya Kikae

Tukiichunguza sanaajadiiya na fasihi simulizi yake, tunapata faida nyingi za kutudhihirishia mengi. Data 1.2.14.1 na 2 ni nyimbo za kuchombezea wanakele. Midundo iliyomo ya kimuziki, mizani ya mpangilio, na sauti za kina zinazokwenda kwa pamoja, ni ushahidi tosha kwamba asasa ya ushairi wetu wa leo wa Kiswahili ni mida ya namna hii.

Data 1.2.13, 1.2.14.3 na 1.2.15.1 na 1.2.15.2 ni baadhi tu ya nyimbo au mida ya paukwani. Nazo zimo katika maumbo maalumu yakijidhihirishia upekee wa dhana ya *mwida* katika sanaajadiiya ya wilaya ya Kusini. Na umbo hili la mwimbo au mwida wa Kiswahili hichi linajionesha lenyewe katika data 1.2.21, 1.2.22, 1.2.24 na 1.2.27. Kwa mfano: Bismillahi Allah ndio ya kwanza... ni umbo hai lililoathiri mianzio yote ya tenzi za Kiswahili zitungwazo na Waswahili kwa kusomwa na Waswahili. Data 1.2.27.2 linaunganisha ukale na usasa kwa kutumia taswira za ndoa na kisomo cha skuli.

Kuna nyimbo fupi fupi zenyenye kurudiarudia maneno, na kuna fupi za ubeti mmoja, nyingine misitari miwili mitatu, nyingine mine lakini kuna nyingine zinazoendelezwa kuimbwa hadi mwimbaji asitishwe na pumzi zake. Hili ni suala la utafiti wa kulichimba hili umbo hadi lichimbuke ili tufahamu mipaka ya mwida na shairi, mwida na utenzi, mwida na tambiko n.k. katika ushairi wa lugha hii ya Kikae.

Paukwa zilizotambwa na watu wazima kwa watoto, zenyenye kusimulia visa na mikasa, nyingi ni zile zinaozoleza hali halisi katika maisha ya waasisi wa utamaduni wa Kikae kutokana na huko makwao barani Afrika walikotokezea. Data 1.2.33 inayowamaliza wanyama wakubwa wakubwa na kumbakiza mnyama mjanja wa Afrika Mashariki - Kibalabala au sungura au Buga inathibitisha matukio halisi ya maisha Kisiwani Unguja. Leo, akionekana mnyama mkubwa ni wa kufugwa ama na watu binafsi au na serikali.

Vitendawili vinapotaja Makka, kufikwa kwa mwendo wa utelezi na kuhusisha fedha, jini na bahari na nazi katika data 1.2.34 ni dhahiri kuwa vinaonesha watu waone kwa macho yao kuwa uswahili-mama ni upwani.

Zimwi anayetajwa sana katika paukwa za Kikae ni zimwi yule yule ambaye kajaa tele katika simulizi za lugha za majirani Bagamoyo, Kisarawe, Handeni n.k. Makame wa Makame, ambaye katika sanajaadiiya ya Wakwere angeitwa Haambiliki, anaoneshwa kuwa ukaidi haufai mbele ya halaiki ya watu. Ama hakika data 1.2.31 ni muhimu sana katika kuwafunda watu ambao hawataki kuambiwa bali hutaka kuona.

2.2 DHABIRI YA MAGUNDUZI

Kwa data iliyopatikanwa na kuchambuliwa kwa haja zetu, yatosha kumpa mtafiti mwanzo mwema wa kutamka kuwa Kikae ni lahaja ya Kiswahili ambayo iko karibu sana na lugha za ukanda wa pwani ya Mrima. Utamaduni wa Kiswahili hiki unadhihirisha utajiri wa utamaduni wa Kiswahili pindi lahaja zote zitakusanya data

za kuonesha uzito wa yaliyopatikanwa. Ama kwa hakika Kiswahili sanifu kitapata pahala pa kujishika vizuri mno kwamba tamaa za ubanangifu hazitapata mwanya wa kupita .

2.3 TANZU ZA UTAMADUNI WA WAMAKUNDUCHI

2.3.1 Wamakunduchi wana lugha yao ambayo ni Kikae au Kimakunduchi (au Kikusini iwapo tunasema hivyo tukiwa tumo Kisiwani Unguja). Lugha hiyo tumeshaikeleza na kudokeza utajiri wake kwa upande wa msamati, fasihi na utamaduni kwa jumla.

2.3.2 Kazi za watu hawa wa Kusini ya Unguja ni pamoja na kilimo (sehemu kadhaa watu hulima maweni), uvuvi, ukwezi, miti ya matunda n.k. ujenzi, biashara, uganga na hasa huo uganga wa mwaka ambaa unaonekana ni wa kipekee sana. Watu wa ukanda wa Mrima wenye jadi za kusherehekea mavuno kwa tambiko na magoma, nao wanayo miganga yao ya kukaga mambo yao ingawa haifanani na ada ya kuoga mwaka. Asasa ya huko nyuma asilini yaweza kuwa moja.

2.3.3 Paukwa zao nyingi zinahusu maisha ya ndoa. Kuna fitina mama wa kambo kwa watoto wa waume zao. Kuna fitina za ukewenza. Kuna kunyang'anyana waume kwa wake. Uzazi umepewa uzito maalumu katika ndoa za Wamakunduchi.

2.3.4 Mithali na misemo mingine imo katika data ya mswada wa Maam Haji Chum.⁹ Misemo hii ni katika jumla ya mafumbo na vijembe vya Kiswahili. Mifano: *kuku mna wana halembewa bwe* (kuku mwenye watoto halengwi jiwe), *kulya nguru si kazi, kazi kumosa* (kula nguru si kazi, kazi ni kumuosha) *mdota asali hadoto umoja* (muonja asali haonji mara moja), *si kiya mna kuche simba* (si kila mwenye makucha ni simba). Katika mafumbo yao, huwa wanasema makubwa na mazito sana. Mfano, zaidi ya hii hapa juu, ni data 1.2.27.3.

2.3.5 Dini ya Kiislamu imetawala vipengele vyote vya maisha ya watu wa wilaya ya Kusini. Kwa kuwa Uislamu haubagui Dini na Siasa, Dini na Kazi, Dini na Starehe n.k. na kwa kuwa wenyeji wote ni Waislamu, kila jambo lao hutangulizwa na Allah, Quran yake, Muhammad (A.M.I.N.) n.k.

2.3.6 Kuhusu vipengele mbalimbali vya maisha ya kila siku, tabia ya Mswhahili daima ni ile ile. Hajitutumui na kujigamba kuwa analo analoliweza. Yeye daima ni mnyonge kwani muweza wa yote yuko Qadiiru na mjua yote yuko Aalim, naye si mwingine bali ni Mwenyezi Mungu.

Mapenzi, watoto wa kike hufundwa, data 1.2.16.1 kuwa kila mwanaume anafaa kuwa mume muhimu ni *kipendacho moyo*. Ujumbe uliojificha katika *mchagua*

⁹ Haji Chum, *Utamaduni wa Watu wa Wilaya ya Kusini-Unguja*. Mswada unaotayarishwa kutolewa kitabu (Mhariri Dkt. T.S.Y. Sengo).

jembe si mkulima na chelewa chelewa utamkuta mtoto si wako ni hadhari tosha ya maamuzi ya Mswahili. Mahusiano baina ya mwanaume na mwanamke na nafasi ya kila mmoja wao ni mambo yaliyowekwa wazi na Qurani na kufafanuliwa na hadithi za Mtume (A.M.I.N.). Anayeyapinga maelekezo hayo, au kuyageuza hata kuyaamini nusu, atajikuta katika moja ya makundi matatu kundi la waasi au wasaliti, kundi la wanafiki na kundi la mashirikina. Kila kundi lina adhabu zake ambazo nazo hazina uficho.

Kwa Mswahili, misingi yote ya maisha imeshawekwa. Hakuna jipyä. Kila linalotokea kwa upande wa magunduzi k.v. makompyuta n.k. ni mambo ambayo yamo katika bongo la Mswahili. Dini yake haina mapindipindi ya kupitwa ni wakati ila wakati hufuata nyendo za Dini ambazo ndizo zinazoendesha dunia na maisha.

Dhana ya heshima imeshika Uswahilini kote. Ina maana pana sana. Inaingiza dhana ya ukarimu, wema, adabu na tabia njema, mwendo mzuri, ibada, kazi n.k. Aliyoyasema Mwana Kupona 1860 bado yana nguvu zile zile Uswahilini kote.

"La kwanda kamati Dini

Pili uwa na adabu

Na ulimi wa thawabu...

La tatu uwa Sadiki

Ushikalo ulithiki...¹⁰

- 2.4 *Naam, kama ni ng'ombe keshaliwa wote kabakia mkia, Sasa tuagane Wenyeji wetu tunaondoka na deni kubwa. Mwajua nyinyi, mja si lolote si chochote, mchechefu wa kumbukumbu na shukurani kabisa hana. Na sisi tu waja. Mtuwie radhi kwa yote. Na sisi pia tu waja. Tusameheane na mji mji wenu karibuni tena. Kwa herini. Karibuni.*

Mila na sanaajadiiya zilizooneshwa na data pamoja na uchambuzi wa data zilizomo katika makala haya, zina umuhimu mmoja mkubwa. Ndizo ushahidi na ithibati ya uhai wa lugha ya Kikae na utamaduni wa Wamakunduchi na wenzao wote wa wilaya ya Kusini Unguja. Kama lahaja hii moja tu imetupa matumaini ya kuwa ni chemchem yenye kina kirefu, hapana shaka ni dhahiri kwamba matumaini kama hayo yatapatikana katika lahaja nyingine pia. Kama hivyo ndivyo, mradi huu wa pamoja, baina ya Taasisi ya Uchunguzi wa Kiswahili Chuo Kikuu cha Dar es Salaam na Idara ya Masomo ya Kiasia na Kiafrika, Chuo Kikuu cha Helsinki, utakuwa, kwa mara ya kwanza katika mapisi ya Kiswahili, umejenga msingi imara sana wa eneo na wa watu waliokizaa Kiswahili na ambao ni hai hadi leo wakiendelea kuilea lugha hii muhimu katika maendeleo ya mja, si katika pwani wala Afrika Mashariki tu bali Afrika na duniani kote.

Kama watu wanavyokwenda mbio Uingereza kwa Kingereza safi na sanifu, Uchina kwa Kichina safi na sanifu n.k ndivyo sasa watu watakavyokuja mbio

¹⁰ Mwana Kupona, "Utendi wa Mwana Kupona". Ktk. Ireri MBAABU (Mhar.), *Utamaduni wa Waswahili*. Nairobi. 1985. Uk. wa 6.

Uswahilini kwa Kiswahili safi na sanifu. Marejeleo ya jitihada zote za kuikuza lugha ya Kiswahili ni lazima yawe Uswahilini - pwani pwani mwa Afrika Mashariki na visiwa vyake. Chuki za kidini na choyo cha kuwakuza Waswahili ni masuala mbali, tuyaache kwa wanasiwa wa hizo dini na kwa watu wenye muhemuko yao. Taaluma komavu hushughulikia kweli kama hii iliyodhihirishwa na kuthibitishwa na data za utafiti wa masikanini na vitabuni.

MAREJELEO

Abeid K.A. 1965.

Sheria za Kutunga Mashairi na Diwani ya Amri. Dar es Salaam: East African Literature Bureau.

Akida H. 1977.

Utamaduni, matumizi na misingi ya lugha ya Kiswahili. **MULIKA** 11, kur. 9-18.

Chiraghdin S. 1974.

Kiswahili na Wenyewe. **Kiswahili** 44:1, kur. 48-53.

Chum H.

Utamaduni wa Watu wa Wilaya ya Kusini-Unguja. (Mswada unaotayarishwa kutolewa kitabu, Mhariri Dkt. T.S.Y. Sengo).

Connah G. 1987.

African Civilization: Pre-colonial cities and states in tropical Africa. An archaeological perspective. Cambridge.

Ladda P.E. (Mhar.) 1982.

Mchango wa Mtwara katika ukombozi Tanzania. Mkoa wa Mtwara.

Mbaabu I. (Mhar.) 1985.

Utamaduni wa Waswahili. Nairobi: Kenya Publishing & Book Marketing Co. Ltd.

Mwana Kupona 1985.

Utendi wa Mwana Kupona. Ktk. Ireri Mbaabu (Mhar.), **Utamaduni wa Waswahili.** Nairobi: Kenya Publishing & Book Marketing Co. Ltd.

Nurse D. na Spear Th. 1985.

The Swahili: Reconstructing the History and Language of an African Society, 800-1500. Philadelphia.

Sengo T.S.Y. 1985.

The Indian Ocean Complex and the Kiswahili folklore: The case of Zanzibarian Tale-Performance. Unpublished Ph.D thesis. Khartoum University.

Shariff I.N. 1988.

Tungo Zetu. Trenton: The Red Sea Press, Inc.